MUHTASARI WA KIKAO CHA PILI CHA BODI YA BARABARA YA MKOA WA RUKWA KILICHOFAYIKA TAREHE 30 MARCHI, 2010 KATIKA UKUMBI WA RDC ULIOPO KATIKA OFISI YA MKUU WA MKOA WA RUKWA.

1.0 MAHUDHURIO:

1.1 Wajumbe waliohudhuria:

1.	Mh. Daniel Ole Njoolay	- Mkuu wa Mkoa	- Mwenyekiti
2.	Bw. Salum M. Chima	- Katibu Tawala (M)	- Katibu
3.	Mh. Thobias M. Sijabaje	- Mkuu wa Wilaya SBA	- Mjumbe
4.	Mh. Joyce W. K. Mgana	- Mkuu wa Wilaya Nkasi	- Mjumbe
5.	Col. J. A. Mzurikwao	- Mkuu wa Wilaya Mpanda	- Mjumbe
6.	Mhe. Frank Mrema	- Meya - Manispaa ys SBA	- Mjumbe
7.	Mhe. David C. Ngalula	- Mwenyekiti wa H/W Nkasi	- Mjumbe
8.	Mhe. Alfred Mwanga	- Mwenyekiti wa H/W ya SBA	- Mjumbe
9.	Mhe. Philip J. Kalyalya	- Mwenyekiti wa H/W Mpanda	- Mjumbe
10.	Mhe. Yasini M. Katampa	- Mwenyekiti wa H/M Mpanda	- Mjumbe
11.	Bw. Lupilya G.S	- Kaimu Mkurugenzi Manispaa SBA	- Mjumbe
12.	Bw. Benjamin O. B	- Kaimu Mkurugenzi HW/SBA	- Mjumbe
13.	Bw. Robert R. Mnkyalla	- Kaimu Mkurugenzi H/W Nkasi	- Mjumbe
14.	Eng. Emmanuel Kalobelo	- Mkurugenzi H/W Mpanda	- Mjumbe
15.	Bw. Henry Haule	- Mkurugenzi wa Mji Mpanda	- Mjumbe
16.	Bw. Baraka H.Mkuyu	- Mhandisi Manispaa S'wanga	- Mjumbe
17.	Bw. Albert S.Kyando	- Mhandisi Mji Mpanda	- Mjumbe
18.	Bw. Joseph Nyamhanga	- MenejaTANROAD Mkoa	- Mjumbe

WASIOHUDHURIA:

1.	Mhe. Mizengo K. Pinda	-Waziri Mkuu na Mbunge Mpanda Mashariki-Mjumbe
2.	Mhe. Dr. Chrisant Mzindakaya	- Mbunge Jimbo la Kwela - Mjumbe
3.	Mhe. Ludovick Mwananzila	- Mbunge Jimbo la Kalambo - Mjumbe
4.	Mhe. Said Arfi	- Mbunge Jimbo la Mpanda Kati - Mjumbe
5.	Mhe. Elietta Switi	- Mbunge wa Viti Maalum (M) - Mjumbe
6.	Mhe. Anna Lupembe	- Mbunge wa Viti Maalum(M) - Mjumbe
7.	Mhe. P. P. Kimiti	- Mbunge Sumbawanga Mjini - Mjumbe
8.	Mhe. Ponsiano D. Nyami	- Mbunge Jimbo la Nkasi - Mjumbe
9.	Mhe. Abdallah Sumry	- Mbunge Jimbo Mpanda Magharibi - Mjumbe

10. Bw. Richard Lobulu -Mhandisi Sekretariat - Mjumbe

WAALIKWA

(a) Wataalam wa Sekretarieti ya Mkoa

1. Bw. Elias M. Msafiri - Katibu Tawala Msaidizi - Huduma za Utumishi na Utawala
2. Bibi E. S. Mfinanga - Katibu Tawala Msaidizi - Huduma za Jamii
3. Bw. S. J. Mundia - Katibu Tawala Msaidizi Huduma za Serikali za Mitaa
4. Bw. W. J. Mnzava - Kaimu Katibu Tawala Msaidizi Maendeleo ya Uchumi
5. Bw. D. E. P. Kilonzo - Kaimu Katibu Tawala Msaidizi Mipango na Uratibu
5. Bw. K. Mahundi - Kaimu Katibu Tawala Msaidizi - Miundombinu
5. Bw. L. J. Kanoni - Katibu Tawala Wilaya ya Mpanda
6. Bw. S. Shillingi - Katibu Tawala Wilaya ya Sumbawanga
7. Bw. Josephat B. Kakuru - Katibu Tawala Wilaya ya Nkasi
8. Bw. A. M. Masse - Mshauri Ustawi wa Jamii Sekretarieti ya Mkoa
10. Bw. P. Mwandumbya - Mwanasheria wa Sekretarieti ya Mkoa
11. Dr. S. R. Kabuma - Mganga Mkuu wa Mkoa
12. Bw. Hamza Mvano - Kaimu Mshauri Kilimo Sekretarieti ya Mkoa
13. Bi. Emmy George - Mhandisi Mshauri Maji Sekeritarieti ya Mkoa
14. Bw. Nicholaus Mchome - Mshauri Maliasili /Mazingira Sekretarieti (M)
15. Bw. Frank J. Maten - Mshauri Maendeleo ya Jamii Sekretarieti (M)
16. Bw. L. M. N Sesemkwa - Mshauri wa Ushirika wa Sekretarieti (M)
17. Bw. Mashalla Samson - DPS wa Mkuu wa Mkoa
18. Bw. Respich Maengo - Kny Mshauri wa Mifugo Sekretarieti (M)
19. G. O. Ouma - Mshauri wa Teknohama Sekretarieti ya Mkoa

AGENDA NA. RRB/ 2010 / 01: KUFUNGUA KIKAO.

Mwenyekiti aliwasili ukumbini saa 3:10 asubuhi kama ilivyokuwa imepagwa. Baada ya hapo Katibu Tawala wa Mkoa Bw. Salum M. Chima, ambaye ndiye Katibu wa Bodi ya Barabara, aliwakaribisha wajumbe wote na kuwapa pole kwa safari kwa wale wote waliotoka nje ya mji wa Sumbawanga. Kisha Katibu alisoma majukumu yaliyo mbele ya kikao cha Bodi ya barabara cha tarehe 30 Machi 2010 kuwa ni pamoja na:-

i. Kuthibitisha Muhtasari wa Kikao kilichopita cha tarehe 19 Oktoba 2009, na kupata taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya kikao hicho.

ii. Kupokea taarifa za utekelezaji wa kazi za Barabara Kuu za Mkoa kutoka TANROAD katika mwaka wa fedha wa 2009/2010.

iii. Kupokea taarifa za utekelezaji wa kazi za Barabara za Halmashauri za Manispaa, Mji na Wilaya Mkoani Rukwa katika mwaka wa fedha wa 2009/2010.

iv. Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti.

Baada ya maelezo hayo Katibu alimkaribisha Mkuu wa Mkoa ambaye ndiye Mwenyekiti wa kikao ili afungue.

Mwenyekiti alifungua kikao kwa kuwakaribisha wajumbe wote na kuwapa pole ya safari kwa wajumbe waliotoka mbali, pia alichukua nafasi kuwataarifu wajumbe kifo cha Bw. Isack Masangula aliyekuwa Kaimu Katibu Tawala Msaidizi Kitengo cha Miundombinu aliyefariki usiku wa kuamkia tarehe 23/02/2010. Aliwaomba wajumbe wasimame kwa dakika moja kumwombea kwa Mungu ili aiweke roho yake mahali pema peponi.

Mwenyekiti alitumia nafasi hii kumshukuru Mhe. Dkt Jakaya Mrisho Kikwete Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumteua Katibu Tawala wa Mkoa. Na kumpongeza Bw. Salum Mohamedi Chima kwa kuteuliwa kuwa Katibu Tawala Mkoa wa Rukwa. Alimkaribisha mkoani Rukwa na kumhakikishia ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi na watendaji wenzake.

Aidha Mwenyekiti alitoa pongezi za dhati kwa Mhehimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumteua Bw. Clement Lujaji aliyekuwa Katibu Tawala Msaidizi Kitengo cha Maendeleo ya Kiuchumi katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ili awe Katibu Tawala wa Mkoa wa Mara. Pia alipongeza kazi nzuri inayofanywa na TANROADS Mkoa kwa kuziweka barabara za Mkoa katika hali ya usafi, kikao kiliagiza TANROADS waendelee kufanya

ukarabati wa barabara ya Sumbawanga – Mbeya,wakati ambao wazabuni wa kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami hawajaanza kazi.

AGENDA NA. RRB/2010 / 02: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA BARABARA KILICHOFANYIKA TAREHE 19 OKTOBA, 2009.

Katibu wa Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Rukwa aliwasilisha Muhtasari wa Kikao cha Bodi kilichofanyika tarehe 19 Oktoba, 2009. Wajumbe walipitia ukurasa baada ya ukurasa na kufanya masahihisho katika ukurasa wa 14 ambapo kwenye hoja ya pili kuna neno "mana" lisomeke maana.

Baada ya masahihisho hayo wajumbe waliuthibitisha Muhtasari wa Kikao cha Bodi ya barabara cha tarehe 19 Oktoba, 2009, kuwa ni kumbukumbu sahihi ya yaliyojadiliwa katika kikao hicho.

AGENDA NA. RRB/2010 / 03: YATOKANAYO NA KIKAO CHA BODI KILICHOFANYIKA TAREHE 19 OKTOBA 2009.

Taarifa ya utekelezaji wa maazimio / maagizo ya kikao cha tarehe 19 Oktoba 2009 yaliwasilishwa na Katibu. Baada ya kupitia azimio moja baada ya jingine, Bodi ilipewa maelezo ya ziada yafuatayo:-

i. Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi iendelee kufuatilia maombi yaliyowasilishwa OWM -TAMISEMI kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Mongamkulu-Korongwe.

   Utekelezaji
   Halmashauri iliendelea kufuatilia maombi hayo kwa kuandika barua ya kukumbushia yenye kumb. Na. NKS/DC/B/20/6/56 ya tarehe 15/02/2010.

ii. Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga waendelee kuitunza barabara ya Mwimbi-Mozi iliyotengenezwa na TANROADS Mkoa wa Rukwa, ili isijifunge tena.

   Utekelezaji
   Barabara ya Mwimbi –Mozi imeingizwa kwenye mpango wa mwaka wa fedha wa 2010/2011 katika kipengele cha "Other road".

iii. Halmashauri ziendelee kushirikiana na Ofisi ya TANROADS Mkoa wa Rukwa katika kutekeleza ujenzi wa barabara za lami zinazoendelea kujengwa.

Utekelezaji

Agizo hilo limezingatiwa kwa Halmashauri ya Mji Mpanda wameshirikiana na Meneja wa TANROADS katika vikao vyote vya kazi za matengenezo ya barabara kwa kiwango cha lami. Kwa upande wa Manispaa ya Sumbawanga huwahawamshirikishi Meneja wa wakala wa Barabara "TANROADS". Wajumbe walipendekeza katika utengenezaji wa barabara za Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga Meneja wa Wakala wa Barabara "TANROADS" ashirikishwe vilivyo.

iv. Wajumbe walimwomba Mwenyekiti aendelee kulifuatilia Suala la ujenzi wa uwanja wa ndege wa Sumbawanga kwa kiwango cha lami.

AGENDA NA.RRB/2010/04:TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA KAZI KATIKA BARABARA KUU ZA MKOA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2009/2010 NA MPANGO WA KAZI NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA WA 2010/2011.

Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Rukwa aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa kazi katika barabara kuu za Mkoa katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, pamoja na Mpango na bajeti ya matengenezo ya barabara kuu za Mkoa na miradi ya maendeleo katika mwaka wa fedha wa 2010/2011.

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa hiyo wajumbe wa Bodi walitoa maazimio yafuatayo:-

(i) Wajumbe waliipongeza TANROADS kwa kuandaa taarifa nzuri na hatua nzuri ya utekelezaji wa kazi katika barabara kuu za Mkoa. Wajumbe waliipongeza Serikali kwa hatua iliyofikia ya ujenzi wa barabara za Sumbawanga - Laela km (96.5) kwa kupata Mkandarasi wa ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

(ii) TANROADS ilipongezwa kwa kazi nzuri waliyofanya kwani hadi kufikia mwenzi Machi 2010 wamefikia asilimia 80% ya kazi za utengenezaji wa barabara. Baada ya majadiliano ya kina, wajumbe walitoa tamko la kuipongeza Serikali kwa hatua nzuri iliyofikiwa ya ujenzi wa barabara mbalimbali Mkoani Rukwa kwa kiwango cha lami na kuipongeza TANROADS kwa kazi nzuri wanazozifanya.

(iii) Wajumbe waliazimia kuwa utengenezaji wa barabara kuu ya Mkutano hadi Sumbawanga, kwa upande wa Rukwa hali si nzuri na inahitaji matengenezo yafanyike katika maeneo korofi.

(iv) Meneja wa TANROADS aliagizwa kuandika barua kuiomba Serikali kufanya mabadiliko ya barabara zile ambazo zilikuwa kwenye mpango wa PMMR

kutoka sumbawanga kupitia Chala hadi Kanazi km (75). Barabara zilizopendekezwa ni kama ifuatavyo:

-Mpanda – Inyonga Konga km (135)
-Nkana- Kala km 68
-Nkundi – Kate hadi Mkangale km 75
Barabara ya Nkundi kupitia Kate hadi Mkangale ilipitishwa kuingia kwenye mpango wa PMMR (*Performance- Based Management and Maintenance of Roads)*.

AGENDA NA. RRB/2010/05: TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA KAZI KATIKA BARABARA ZA HALMASHAURI ZA WILAYA, MANISPAA YA SUMBAWANGA NA MJI MPANDA KATIKA MWAKA WA FEDHA WA 2009/10 NA MIPANGO YA KAZI NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA WA 2010/2011.

Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri Wilaya za Sumbawanga, Nkasi na Mpanda, Mkurugenzi wa Manispaa ya Sumbawanga na Mkurugenzi mtendaji wa Mji wa Mpanda waliwasilisha taarifa za utekelezaji wa kazi katika barabara zilizo chini ya Halmashauri zao.
Baada ya kuwasilisha taarifa wajumbe walijadili kama ifuatavyo:-

(i) Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga.

- Wajumbe waliomba ufafanuzi kama barabara ya lami kutoka maeneo ya Mkoani kwenda Ikulu na Kristu Mfalme kwa nini haijafika Hospitali ya Dr.Atman. Mhandisi wa Manispaa ya Sumbawanga alithibitisha kuwa ni kweli barabara haijatengenezwa kufika Hospitali ya Dr.Atman, kwa sababu Mkandarasi wa barabara za Manispaa ya Sumbawanga amesimama kutokana na mvua zinazoedelea kunyesha. Mkandarasi ataanza kazi tena mwezi Mei kukamilisha kazi za barabara zilizobaki ambazo zipo kwenye mkataba.

- Pia washiriki walitaka kujua kama lami iliyowekwa kwenye barabara za Manispaa ya Sumbawanga kama kuna tabaka jingine litawekwa, Mhandisi wa Manispaa ya Sumbawanga alisema hakuna pale ni mwisho kwani ujenzi wa barabara hizo umekamilika kwa asilimia 90%.

- Wajumbe hawakukubaliana na utengenezaji wa barabara za lami. Vilevile kwenye maunganisho ya barabara kuu na zile zinazotengenezwa kwa kiwango cha lami, barabara hizo hazina usawa “uniformity” na

barabara kuu kwa sababu ya kutounganisha vizuri na kusababisha vilima kati ya barabara hizo na barabara kuu kuwa chini na zile zinazotengenezwa kuwa juu .

- Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga iliagizwa kurekebisha maungio ya barabara hizo.

- Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga ilishauriwa kutengeneza barabara ya Mkuu wa Wilaya (Nyumbani kwa Mkuu wa Wilaya – Bomani) hata kwa kuwaomba Makandarasi ambao wamepewa kazi kubwa kutoa msaada angalau wa kukwangua barabara hii.

- Mwenyekiti alipendekeza kutoa Tamko kuhusu barabara za lami za Manispaa ya Sumbawanga. Baada ya majadiliano wajumbe walikubaliana kwamba, kwa kuwa timu imeundwa kufutilia ujenzi wa barabara hizo haitakuwa vema kutoa Tamko kuhusu barabara hizo.

(ii) Halmashauri ya Mji wa Mpanda.

Taarifa ya Halmashauri ya Mji wa Mpanda ilipokelew. Wajumbe waliipongeza Halmashauri kwa kushirikiana na wakala wa barabara “TANROADS” katika ujenzi wa barabara za lami za mji Mpanda. Aidha, Meneja wa TANROADS alisema kwa upande wa Mjini Mpanda wanashirikiana vema katika ujenzi wa barabara za lami. Wajumbe waliagiza Halmashauri ya Manispaa Sumbawanga iende kujifunza jinsi ya kutengeneza barabara za lami kwa Halmashauri ya Mji Mpanda.

(iii) Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga.

Taarifa ya Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga iliwasilishwa na hakukuwa na hoja yoyote kutoka kwa wajumbe. Aidha ombi maalum la kuomba kuongezewa fedha za Bajeti kwa ajili ya ukabarabati wa barabara ziongezwe kwa mwaka wa fedha 2010/2011 liliwasilishwa na kukubaliwa.

(iv) Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda.

Taarifa ya Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda iliwasilishwa na wajumbe waliipongeza Serikali kwa ukarabati mzuri wa barabara.

(v) Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi.

Taarifa ya Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi iliwasilishwa na wajumbe hawakulidhika na ukarabati wa barabara za Halmashauri ya Nkasi, Mwenyekiti alishauri Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi kutangaza Zabuni.

AGENDA NA. RRB/2010/06: TAARIFA YA SUMATRA.

Taarifa ya SUMATRA iliwasilishwa na kupongezwa na wajumbe kwa kazi nzuri zinazofanywa na SUMATRA katika Mkoa wetu. Aidha wajumbe walitumia fursa hii kuwaomba Maafisa wa SUMATRA waruhusu magari ya mizigo kubeba abiria ili kutatua tatizo la uhaba wa usafiri hasa kwa vijijini.

- Kutokana na uhaba wa vyombo vya usafiri wajumbe waliiomba SUMATRA kuwashawishi wawekezaji ili waje kuwekeza katika ziwa Tanganyika kwani mpaka sasa hakuna usafiri wa uhakika katika ziwa hilo.

- Kikao kilitoa mapendekezo ya kuishauri Serikali kuwa na mamlaka nyingine ya kushughurikia Bandari. Aidha iliazimiwa katika kikao cha Bodi ya barabara kijacho waalikwe Mamlaka ya bandari.

AGENDA NA.RRB/2010/07: MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI.

Hoja ambazo ziliwasilishwa katika agenda hii ni:-

(1) Halmashauri ziandae mpango wa kujenga madaraja katika barabara zetu ili zipitike wakati wote wa masika.

(2) Mwenyekiti wa CCM (M). Alipongeza kazi ya ukarabati wa barabara inayofanywa na Serikali. Alisema hadhi ya Chama Cha Mapinduzi imepanda kutokana na kazi nzuri inayofanyika. Aliitaka Serikali kuongeza kasi ya ukarabati wa barabara bila kupunguza.

(3) Wajumbe hawakuridhishwa na ujenzi wa Gati la kipili mbali na Ofisi za Polisi, T.R.A na Uhamiaji ambazo ni Taasisi muhimu zinazotoa huduma kwa wananchi, hivyo Wajumbe waliomba Gati hilo lijengwe karibu na Taasisi hizo. Katika kusisitiza jambo hili Wajumbe walimwomba Mwenyekiti kupitia mamlaka aliyonayo awaandikie barua Mamlaka ya Bandari Tanzania ili iridhie ujenzi wa Gati karibu na Taasisi hizo kama ilivyokuwa zamani na kusitisha ujenzi wa Gati sehemu ya mbali.

(4) Ili kutunza barabara zetu Wajumbe waliagiza Halmashauri zitunge sheria ndogo ndogo kwa ajili ya wanaopitisha mifugo barabarani.

AGENDA NA. RRB/2010/08: KUFUNGA KIKAO.

Mwenyekiti alifunga kikao kwa kusisitiza kuwa, katika kutekeleza na kusimamia ujenzi wa barabara,viongozi wa Serikali Kuu na Halmashauri katika ngazi zote Mkoani Rukwa, wakawaelimishe wananchi wanaoishi katika maeneo ambayo barabara zinatengenezwa ili kusaidia Makandarasi wa barabara waweze kutekeleza kazi zao kwa ufanisi na utulivu. Alitaja mambo manne ya kwenda kuwaelimisha/kuhamasisha wananchi kama ifuatavyo:-

(i) Kutumia fursa za ajira zilizopo wakati wa ujenzi wa barabara.

(ii) Tahadhari dhidi ya mambukizi mapya ya VVU/UKIMWI kutokana na mwingiliano wa jamii mbalimbali wakati wa ujenzi barabara.

(iii) Kutoa elimu kwa wananchi wa Mkoa wa Rukwa, kuchukua tahadhari wanapopata wageni wengi wanaotaka kununua ardhi ili wasiuze ovyo ardhi waliyonayo.

(iv) Wananchi wahamasishwe kuwa walinzi wa mali za Makandarasi katika maeneo yao ili mali na vifaa vya Mkandarasi visiibiwe.

Mwisho aliwashukuru wajumbe kwa mchango wao na kufunga kikao rasmi saa 6.48 mchana.

U M E T H I B I T I S H W A

Salum M. Chima

MWENYEKITI **KATIBU**

…… **……**

TAREHE:…… **TAREHE:……**